

Watoto 270 wenye ualbino waugua utapiamlo

■ Stephen Kidoyayi, Shinyanga

WATOTO 270 wenye umri wa chini ya miaka mitano wanaoishi katika kituo cha walemaru wa ngozi cha Shule ya Msingi Buhangija wilayani hapa, wamekumbwa na utapilamlo kutokana na kula mlo wa aina moja kila siku.

Mkuu wa Shule hiyo, Selemani Kipanya alifichua hayo juzi, baada ya kituo hicho kutembelewa na wadau ili kushirikiana na watoto hao kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika.

Alisema watoto wa kituo hicho wapatao 431 wakiwamo 321 wenye ulemavu wa ngozi, wasioona 40 na wasiosikia 69 kati yao 270 wakiwa na umri chini ya miaka 12 wamekumbwa na ugonjwa huo, kutoka na kula ugali, walii kwa maharage kila siku.

Siku hiyo watoto hao walitembelewa na walimu wanawake wa mkoa wa Shinyanga, walioamua kupika chakula na kula na watoto hao na kuonesha upendo kwao.

Akizungumza kwa niaba ya walimu hao, Neema Obedi alisema waliamua kupika chakula kituoni hapo na kula pamoja kutokana na watoto hao kuwa sawa na wafungwa ambaeo hawapati upendo wa wazazi na kubaki kwenye eneo linalofanana na chumba.

"Sisi ni wazazi na walezi na watoto hawa, tunawaona kama watoto wetu, tumeferijika kushirikiana nao leo na hii itakuwa endelevu kwani watoto wamekaa kama wametengwa na jamii, na wamefungiwa kwenye chumba na wadau hawawaoni ili kuwasaidia na kuwapa upendo kama watoto wengine," alisema Obedi.

Walichangia Sh milioni 2 za kununua chakula, vifaa vya darasani, nguo za watoto wa kike na dawa za tiba, mafuta ya kujipaka, mifagio ya chooni na vifaa vya jikoni.

Siku hiyo pia wafanyakazi wa Halmashauri ya Ushetu, Kahama walifika kituoni hapo na kula pamoja baada ya kupika hapo hapo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Isabella Chilumba alisema waliamua kufika kituoni hapo,



Mhadhiri wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Apium Chengula (kulia), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam (hawapo pichani), wakati akitoa majumuisho yaliyofikiwa katika jana Kongamano la kitafifa na kimataifa liliiloandalialiwa na chuo hicho. Kushoto ni Mratibu wa Mpango wa Shirika lisilo la kiserikali la Konrad Adenauer Stiftung (KAS), Richard Shaba. (PICHA NA DOTTO MWAIBALE)

kutokana na kuwa na watoto waliotoka halmashauri hiyo ili kushirikiana nao siku hiyo maalumu.

Alisema wafanyakazi wa Halmashauri hiyo walichangia Sh 588,000 kwa ajili ya chakula na vinywaji na Ofisi ya Mkurugenzi

ikachangia Sh milioni moja zilizonuu chakula huku Shirika la Msalaba Mwekundu likichangia Sh milioni 1.7 kwa ajili ya vitambulisho vya Bima ya Afya kwa watoto tisa waliotoka halmashauri hiyo na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Asilimia 70 ya makazi Arusha yamejengwa kiholela

■ Mwandishi Wetu, Arusha

TAKWIMU zinaonesha kuwa asilimia 70 ya makazi ya Jiji la Arusha yamejengwa kiholela. Hayo yamebainishwa injini hapa juzi katika mkutano wa kujadili mpango mkakati wa kuliweka Jiji la Arusha kuwa kwenye mpangilio safi.

Katika mkutano huo ilielezwa kuwa ramani ya mpangilio. wa jiji hilo inatarajiwaa kukamilika Agosti, mwaka huu na kwamba tayari madiwani wameshapatiwa mafunzo kuhusiana na mpango mji huo.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Daudi Ntibenda alisema mpango mji huo umekusudia kuweka sawa sura ya jiji hilo kupidia ubainishaji wa maeneo ya ujenzi, kupendekeza mpangilio wa miundombinu na mpangilio wa mji ambaeo utachangia kuyafikia malengo ya Mpango Thabiti wa Matumizi ya Ardhi wa mwaka 2035.

"Tumeridhishwa na majadiliano kuhusu mpango mji na miundombinu ya usafiri, tunapofanya kazi pamoja ya kuwa na mpangilio wa Jiji la Arusha 2,035. Nia yetu ni kuufanya mji wa Arusha kuwa wa kisasa na wa kiuchumi," alisema Ntibenda. Awali, ramani ya mpangilio wa jiji hilo ulijumuisha eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 278, lakini mpango mpya unatarajiwaa kujumuisha eneo jipya la

Bodi Bandari vahimizwa

Mawakili wa Serikali wamwekeea